

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MADINI



### KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)



#### NAFASI ZA MAFUNZO KWA NGAZI YA CHETI

Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) kinatangaza nafasi za mafunzo ya muda mfupi (*Short Course*) katika fani ya **ukataji na usanifu wa madini ya vito** (*Lapidary training course*), **Utambuzi wa madini ya vito** (*Gem Identification*), mafunzo katika **fani ya usonara** (*Introduction to jewelry*) pamoja na mafunzo ya muda mrefu ya **diploma in Gem & Jewellery Technology**.

Mafunzo hayo yatatolewa katika Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC), kilicho chini ya Wizara ya Madini. Kituo kipo Jijini Arusha katika barabara ya Themu karibu na Ofisi ya Madini Arusha.

#### **A. MAFUNZO YA MUDA MFUPI**

##### **Sifa za Mwombaji:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea mwenye kufaulu masomo manne kwa angalau alama D.
- Mafunzo ni kwa jinsia zote na umri wowote.

##### ➤ **Ukataji na ung'arishaji wa madini vito**

###### **i. Muda wa Mafunzo: Miezi 6**

Ada ya Mafunzo: **Tshs 1,100,000/=**

Mafunzo yataanza mwezi **Januari 2019**,

###### **ii. Muda wa Mafunzo: Miezi 3**

Ada ya Mafunzo: Tshs 650,000/=

Mafunzo yanatolewa wakati wowote

##### ➤ **Fani ya usonara** (*Introduction to jewelry*).

Muda wa Mafunzo: **Miezi 3**

Ada ya Mafunzo: **Tshs 900,000/=**

Mafunzo yataanza mwezi **Januari, 2019**

##### ➤ **Utambuzi wa madini ya vito** (*Gem identification*)

Muda wa Mafunzo: **Miezi 3**

Ada ya Mafunzo: **Tshs 550,000/=**

Mafunzo yataanza mwezi **Januari, 2019**

## **B. MAFUNZO YA DIPLOMA IN GEM & JEWELLERY TECHNOLOGY**

### **Sifa za Mwombaji:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea mwenye kufaulu masomo ya Hisabati na Kiingereza kwa angalau alama D na masomo mengine yoyote mawili.
- Mafunzo ni kwa jinsia zote na umri wowote

Muda wa Mafunzo: **Miaka 3**

Ada ya Mafunzo kwa mwaka: **Tshs 1,500,000/=**

Mafunzo yataanza mwezi **March, 2019**

### **MUHIMU**

**Kituo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa namba ya usajili REG/SAT/033 kutoa mafunzo ya diploma.**

### **Jinsi ya Kuomba**

- Jaza fomu ya maombi ukiambatisha nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea, cheti cha kuzaliwa; kitambulisho cha Taifa au Mpiga Kura au Leseni ya Udereva.
- Fomu inapatikana katika Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) na Ofisi zote za Madini au tembelea tovuti yetu **www.tgc.ac.tz**
- Ada ya maombi ya **Tsh 10,000/=** isiyorudishwa. Mwombaji atalipia ada ya maombi kupitia Benki ya NMB, Akaunti namba **40801000074** yenye jina la **Tanzania Gemological Centre** na kuwasilisha *Bank Pay in Slip* (BPS) kwa ajili ya kupata fomu.

Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba: **0756-205028** au **0752-957914**

Tuma maombi pamoja na viambatisho kwa:-

**Mratibu,**

**Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC),**

**S.L.P. 119,**

**ARUSHA.**